



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA WIZARA
YA VIWANDA NA BIASHARA**



WAKALA WA USAJILI WA BIASHARA NA LESENI

TAARIFA KWA UMMA

06.09.2021

KUHAMA KWA OFISI ZA WAKALA WA USAJILI WA BIASHARA NA LESENI (BRELA)

Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) inapenda kuutaarifu umma kuwa, Ofisi zake zilizokuwa kwenye Jengo la Ushirika, Mtaa wa Lumumba Jijini Dar es Salaam zimehamia kwenye Jengo lililokuwa Makao Makuu ya Jeshi la Magereza lililoko kwenye makutano ya Barabara ya Sokoine na Mtaa wa Shaaban Robert, Wilaya ya Ilala Mkoa wa Dar es salaam, kuanzia tarehe 1 Septemba 2021.

Kwa taarifa hii umma unafahamishwa kuwa, huduma za BRELA zinazohitaji mtu kufika katika ofisini zake sasa zitakuwa zinatolewa katika Ofisi hii mpya.

Uhamaji huu una lengo la kuongeza tija na ufanisi katika kutoa huduma bora, hivyo tunaomba radhi kwa changamoto zozote zinazoweza kujitokeza, pia kuwa wavumlivu kwa usumbufu wowote utakaotokana na mabadiliko haya.

Imetolewa Na;
Kitengo cha Habari na Mawasiliano

BRELA House, Sokoine Drive and Shaaban Robert Street, P.O Box. 9393, Dar Es Salaam, Telephone: +255-22-2181344, 2180113, 2180141, 2212800, fax: +255-22-2180371, E-mail: ceo@brela.go.tz, usajili@brela.go.tz, Website: www.brela.go.tz
